

Dhima ya Kamusi Katika Kubainisha Matumizi ya Vihusishi (Mfano: Kihusishi KWA)¹

ALBINA R. CHUWA

University of Dar es Salaam, Tanzania

Miongoni mwa madhumuni muhimu ya kamusi ni kumsaidia mtumiaji wa kamusi kujua maana za maneno, pamoja na matumizi halisi ya maneno hayo. Kwa hali hiyo maneno yanayopata kipaumbele cha kuingizwa katika kamusi ni yale yanayowakilisha dhana fulani, yaani yenye maana leksika, katika lugha. Landau (1984: 120), katika kufafanua maana leksika anataja nduni mbili muhimu. Ya kwanza ni kategoria ya neno (genius), na pili ni kile kitu kinachotofautisha neno hilo na maneno mengine yaliyomo katika kategoria moja (differentia). Pamoja na nduni hizi mbili lipo sharti lisemalo kwamba maana leksika itolewayo inaweza kutumika kama kabadala cha neno linalohusika katika tungo mbalimbali. Yapo maneno kadhaa ambayo sharti hili linashindikana kiutekelezaji, kwa mfano istilahi. Pamoja na maneno haya tunajua wazi kuwa lugha nyingi pia zina vineno² ambavyo havikamilishi masharti mawili yaliyobainishwa hapo juu, kwa maana ya kwamba havina dhana dhahiri ambayo inaweza kuvitofautisha na vineno vingine vilivyomo katika kategoria moja, na wala havina vabadala vinavyoweza kuviwakilisha katika tungo. Lakini, pamoja na upungufu huu, mchango wa vineno hivi katika lugha ni muhimu kwa vile vinashirikiana na maneno yenye maana leksika katika kukamilisha tungo mbalimbali za lugha inayohusika. Kwa mujibu wa Zgusta (1971: 241) vineno hivi havipaswi kusahaulika katika kamusi, kwani pamoja na kwamba haviwakilishi dhana yoyote utendaji wake una nafasi kubwa katika lugha.

Katika warsha ya kanda juu ya kusahihisha Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS) iliyoandaliwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, (16-29/8/1993), Prof. A.M. Khamisi alitoa makala yaliyoitwa 'Taarifa za Kisarufi Katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu', na moja ya pendekezo lake lilikuwa, kuwepo na 'uainishaji wa vihusishi kisarufi na kimaana na kuvipa hadhi ya vidahizo' (uk. 16). Pendekezo hili lina umuhimu mkubwa katika kurekebisha yale yanayoelekea kuleta utenge katika matumizi ya Kiswahili. Vipo 'vineno' kadhaa ambavyo vimejikuta vimerundikwa chini ya kategoria moja kwa kukosa uainishaji sahihi wa kisarufi. Kwa mfano kategoria za kiunganishi, imebebebwazwa mzungo mkubwa wa vineno ambavyo

¹ Makala haya yametolewa katika kongamano 8 la 'Swahili-Kolloquium Bayreuth', tarehe 26 na 27 Mai, 1995.

² vineno katika makala haya limetumika kuwakilisha vihusishi, kwa mfano *na, kwa* n.k. ambavyo vinadaiwa kuwa havina maana leksika; maneno ni yale yenye maana leksika.

kimatumizi havisadifu kategoria hiyo, mathalani vineno vinavyoundwa kwa -a unganifu (ya, na, vya, kwa n.k.). Maneno mengine kwa mfano, baada, kati, mbele, nyuma n.k. yameingizwa katika kategoria za kielezi, na nomino huku yakisahaulika yanapotumika kama kiambata thabiti³, kwa kushirikiana na -a unganifu, kwa mfano, baada ya, kati ya, mbele ya, nyuma ya n.k. katika kategoria ya kihusishi.

Baada ya maandiko mbalimbali kuhusu Kiswahili, kama vile Sarufi ya Maumbo ya Kiswahili, iliyotayarishwa na Kapinga (1983), kuna haja ya kurekebisha kamusi za Kiswahili ili zichukue dhima ya kurekebisha yale yanayojitokeza kutokana na maandishi haya, hasa kwa kuzingatia umuhimu wa vineno hivi katika lugha.

Nia ya mada hii, ni kuangalia kineno *KWA* kwa kuzingatia matumizi yake katika lugha, na kujaribu kupendekeza jinsi kamusi za Kiswahili zinavyoweza kushiriki katika kukidhihirisha kineno hiki katika kategoria zake, yaani kama kiunganishi na kihusishi, na kukitolea maana au maelezo yanayosadifu kutokana na matumizi yake katika tungo mbalimbali za Kiswahili. Ni jambo linalokubalika kuwa maana za vineno, pamoja na maneno ambayo yameambuliwa maana za kileksika, ziorodheshwe kufuatana na matumizi ya maneno hayo katika tungo (Zgusta 1971: 258).

Kwa kipindi kirefu wanaleksikografia wa kamusi za Kiswahili wamekuwa wakivifutika pembeni vineno ambavyo vinadhaniwa kuwepo katika lugha ili kusaidia sintaksia tu, kwa vile havikuonekana kuwa na maana leksika ya moja kwa moja. Vineno hivi pia, wakati wa kuviainisha katika kategoria za kisarufi, vimekuwa vikifananishwa na maneno ya lugha za kigeni, kwa mfano Kiingereza, na kupangwa chini ya kategoria ya kiunganishi, bila kutafakari kama kweli vineno vyote hivyo vinafanya kazi ya kuunga vipashio katika tungo vilimotumika. Kwa mfano *KWA* limeingizwa na kubainishwa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS)* (1981: 141) kama kiunganishi, bila shaka kwa kufuatia pia neno hilo lilivyoainishwa katika *Standard Swahili-English Dictionary* ya Johnson (1939: 233). Lugha nyingi ambazo historia yake ya leksikografia si ya zamani zimejikuta zikiainisha sarufi yake kwa kuifananisha na moja ya lugha ambazo tayari zilishajikita katika uainishaji sarufi. Japo si wazo potofu, lakini kuna umuhimu wa kubadilisha pale ambapo mifumo ya lugha hizi zinazohusishwa hazikubaliani (Zgusta 1971: 126).

Tunapochukua kineno *KWA* kilivyoainishwa kama kiunganishi katika kamusi ya *KKS*, na kuangalia matumizi yake katika lugha tunaona kuwa zipo tofauti za kimsingi zinazotokana na uhusiano unaojidhihirisha kati ya vipashio vilivyohusishwa katika tungo hizo. Kwa mfano, tukichambua maana tano zilizo rodheshwa chini ya kidahizo *KWA* katika *KKS* tunapewa mifano ya tungo zifuatazo hapa chini:

1. Amempiga kwa fimbo.
2. Amekwenda kwa siri.
3. Umekwenda kwa nani?

³ Nawashukuru Ridder Samson na Barwani Sheikh Sauda kwa majadiliano yaliyonifanya nibadili neno *tisti* nililotumia katika makala ya mwanzo, kuwa *thabiti* katika makala haya.

4. Wamefungana mabao matano kwa mawili; shilingi kwa ya pili (nh).
5. Amekula wali kwa kuku (KKS: 141).

Tofauti ambazo zimejitokeza katika mifano minne ya mwanzo iliyotolewa ili kubainisha maana mbalimbali za *KWA*, zinadhihirisha wazi kuwa *KWA* hakiunganishi vipashio vilivyomo katika tungo hizo. *KWA* kinaonyesha uhusiano uliopo kati ya kiima na yambwa kwa kuhusishwa na kitenzi kilichotumika, mara nyingine kikionyesha namna tendo lilivyotekelezwa. Kwa mfano, katika tungo zilizonukuliwa hapo juu (1) *KWA* kinaashiria kifaa kilichotumika katika utekelezaji wa tendo; (2) *KWA* kinaashiria jinsi tendo lilivyofanyika; (3) *KWA* kinaashiria mahali palipoendwa; na (4) *KWA* kinatofautisha mabao yaliyofungwa na timu zilizohusika. Maana ya tano iliyotolewa chini ya *KWA* ndiyo pekee ambayo inasadifu kama kiunganishi.

Kumbe kinachojitokeza hapa si kushindwa kwa KKS kubainisha maana tofauti za matumizi ya *KWA*, bali ni kushindwa kubainisha *KWA* katika kategoria zinazosadifu matumizi yake.

Tukijaribu kuchukua kamusi nyingine ya Kiswahili, *Kamusi ya Maana na Matumizi* (KMM) iliyotayarishwa na S. Bakhressa (1992) na kuangalia ufafanuzi uliotolewa kwa kidahizo *KWA* tunakumbana na yafuatayo. Kwanza kabisa matumizi ya kineno hicho yameainishwa kwa tungo sita (a - f). Mifano iliyo chini ya (a), (b) na (c - sehemu ya kwanza ya tungo: tungo (c) kama inavyoonekana hapo chini inatumia *KWA* kwa namna mbili tofauti), inaweza kuwekwa katika kundi moja na mfano uliotolewa na KKS chini ya namba 1, yaani inaonyesha jinsi tendo lilivyotekelezwa yaani;

- a. Nilisafiri *KWA* basi mpaka kwetu mashambani.
- b. Iandike barua *KWA* kalamu.
- c. Walikwenda sare *KWA* kufungana...

Sehemu ya pili yaani '...kufungana bao moja kwa moja' inaweza kuwekwa pamoja na maana iliyotolewa chini ya namba 4a katika KKS, yaani 'wamefungana mabao matano kwa mawili'.

Mfano uliotolewa na KMM chini ya herufi (d) unahusu matumizi maalumu, kwani *KWA* ni sehemu ya kiambata thabiti ambapo maana ya tungo inapatikana kwa kuangalia kiambata thabiti kwa pamoja, bila kukigawa katika maana changilizi za vipashio vinavyohusishwa. Mfano huu unaweza kufananishwa na ule uliotolewa katika KKS chini ya namba 4, ukifuatiwa na kifupisho (nh) kwa maana ya nahau, kama inavyonukuliwa hapa chini:

- d. (KMM) Nilikuwa nikimdai pesa, naye aliiweka saa yake rehani kwangu: tukalipana *mkono kwa mkono*.
- 4b. (KKS) *shilingi kwa ya pili* (nh).

Mfano uliopo katika KMM chini ya herufi (e) unaweza kuwekwa kundi moja na ule wa 3 katika KKS - mifano hii inaonyesha mahali palipoendwa.

- e. (KMM) Nitakwenda *KWA* Juma leo kuongea naye.
3. (KKS) Unakwenda *KWA* nani?

Mfano wa mwisho katika KMM unafanana na ule uliopo chini ya namba 5 ya KKS, ambao unaonyesha kategoria ya kiunganishi, tofauti na kategoria iliyowakilishwa katika mifano iliyotangulia.

- f. (KMM) Nikiwa nazo pesa hula wali *KWA* kuku (KMM 1992: 193).
5. (KKS) Amekula wali *KWA* kuku.

KWA kina matumizi mengi muhimu katika lugha ambayo hayajapatiwa nafasi katika kamusi, na wala kubainishwa wazi katika maandishi ya lugha. Kupata umahiri wa lugha ni pamoja na kujua matumizi mbalimbali ya vineno hivi ambavyo mzawa wa lugha anaviona ni vya kawaida mno, na kwa hali hiyo, havistahili kumshughulisha mchunguzi wa lugha. Kapinga (1983: 186) ameorodhesha makundi sita ambamo *KWA* kinapotumika kinaeleza aina tofauti ya uhusiano kati ya vipashio vinavyotumika. Katika makundi haya limesahaulika kundi la viambata thabiti, ambamo ndani pia tunaweza kuingiza vitu kama nahau na methali. Ni dhahiri kuwa viambata hivi haviwezi kuingizwa pamoja na maelezo yake yote chini ya kidahizo *KWA* (kama tutafuata kanuni ya kuingiza viambata chini ya kipashio kamili tu - yaani chenye maana leksika), ila, kanuni ya urejeleaji inaweza kutumika ili viambata hivi viorodheshwe chini ya *KWA* na kupewa maelezo kamili chini ya mojawapo ya vipashio vikuu vya kiambata kinachohusika.

Kwa kuongezea makundi sita yaliyotolewa na Kapinga ningependekeza kundi la 7 (saba) ambalo lingebeba viambata thabiti, miongoni vikiwemo pia nahau na methali. Jambo hili ni muhimu kwa sababu tunapomfikiria mfasiri wa lugha au mwanafunzi wa lugha tunashindwa kujua ni kwa njia gani zaidi anaweza kupata haya matumizi maalumu ya *KWA*. Hapa chini imeorodheshwa mifano michache pamoja na tafsiri zake kwa Kiingereza ili kuonyesha umuhimu wa viambata hivyo kupatiwa nafasi katika kamusi za Kiswahili.

- | | |
|------------------------|--|
| a. kwa desturi | <i>naturally, usually, generally</i> |
| kwa hiari | <i>voluntarily</i> |
| kwa hiyo/hivyo | <i>so, in that case</i> |
| kwa kawaida | <i>usually, generally, naturally</i> |
| kwa makusudi | <i>intentionally</i> |
| kwa nini | <i>why</i> |
| b. -enyewe kwa -enyewe | <i>by oneself</i> |
| mara kwa mara | <i>often</i> |
| moja kwa moja | <i>directly, permanently; one by one</i> |
| papo kwa papo | <i>instantly</i> |
| c. kwa ajili -a | <i>for (the sake of)</i> |
| kwa hisani -a | <i>for (the sake of); with apology</i> |

kwa sababu (-a)	<i>because (of)</i>
kwa madhumuni -a	<i>for the purpose of</i>
d. kwa hali na mali	<i>morally and materially</i>
kwa mapana na marefu	<i>in great detail</i>
kwa sauti moja	<i>in unison, together</i>
e. ana kwa ana	<i>face to face</i>
bega kwa bega	<i>together</i>

Tunapoangalia mifano ya viambata vilivyoorodheshwa hapo juu (a) - (e), tunaona kwamba makundi hayo yamepishana katika kiwango cha uribiti kutokana na jinsi *KWA* kilivyoshirikiana na vipashio vingine katika kuunda viambata hivyo. Viambata hivi tunaweza kusema kuwa vipo kati ya viambata huru na viambata thabiti. Kwa mfano katika kundi (a) kila kipashio kinashiriki katika kuchangia maana inayopatikana. Lakini tunapofikia makundi (d) na (e) tunaona kuwa vipashio vinashirikiana kuunda maana iliyo tofauti na maana ambazo zingepatikana kwa kuangalia maana ya kila kipashio kilichoshirikishwa. Viambata hivi kama vinavyojidhihirisha hapa vinatumika katika miktadha ambayo si rahisi kwa mwenye kujifunza Kiswahili kuvijua bila msaada wa aina fulani. Kimbilio la kwanza la mwenye kutaka kujua maana au matumizi yake ni kwenye kamusi. Lakini tukijaribu kuchunguza tunaona kuwa kamusi za Kiswahili bado hazijazingatia swala la viambata vya aina hii, na pale ambavyo vinaorodheshwa, mara nyingi vinapatikana bila maelezo ya kutosheleza na wala mifano ya matumizi.

Tukizingatia maelezo yaliyotolewa tunaweza kuafikiana kwamba vineno hivi si kwamba havina maana leksika, ila maana zake haziwezi kuelezeka kwa kufuata mfumo wa utoaji maana wa maneno ya kawaida katika lugha. Maana zake zinaelezeka kwanza kwa kubainisha kategoria zake, na pili kwa kueleza wajibu vinavyotekeleza katika muundo wa sentensi (Landau 91-2). Kwa vile makala haya ni kama kichocheo cha kujaribu kupata mchango wa namna ya kushughulikia vineno hivi ambayo vipo katika lugha na ambavyo kwa muda mwingi vimekuwa havijatazamwa kwa undani, ningependekeza kwanza kineno *KWA* kiingizwe katika kamusi kikiwa na maelezo yanayosadifu matumizi yake. Kionyeshwe katika sehemu tatu, yaani (1) kama kategoria ya kiunganishi (2) kama kategoria ya kihusishi. Chini ya kila kategoria mifano michache itolewe ili kubainisha matumizi yake sahihi. Baada ya kategoria hizi mbili, (3) yatolewe maelezo mafupi kuonyesha kuwa kineno hiki *KWA* kinatumika pia katika uundaji wa viambata thabiti. Viambata hivi viorodheshwe na kila kimoja kirejelewe katika moja ya vipashio vyake vikuu. Chini ya vipashio hivi ndipo viambata hivi vinaweza vikatolewa maana pamoja na mifano yake ya matumizi. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumempunguzia mjifunzaji Kiswahili adha ya kurejea katika kitabu cha sarufi kila anapokutana na tatizo la aina hii.

Kwa mfano kidahizo *KWA* kinaweza kikapewa umbo lifuatalo katika kamusi ya Kiswahili:

KWA [A] *ku*⁴ hutumika kuonyesha uhusiano kati ya vitu viwili au zaidi vinavyokwenda pamoja: amekula wali *KWA* kuku.

[B] *kh*⁵ (1) hutumika kuonyesha kifaa/chombo kilichotumika: amesafiri *KWA* gari; alimpiga *KWA* jiwe (2) hutumika kuonyesha mahali palipoendwa: amekwenda *KWA* dada; ametoka *KWA* wazazi (3) hutumika kuonyesha sababu: alihudumiwa *KWA* hisani yako; walikufa *KWA* njaa, (4) hutumika kuonyesha mahali jambo lilipotukia: aliiba *KWA* mwenyeji wake; anaishi *KWA* mjomba, (5) hutumika kuonyesha jinsi jambo lilivyotendeka: alilia *KWA* huzuni; tuliondoka *KWA* hiari yetu wenyewe, (6) hutumika kuonyesha tofauti ya mambo mawili: walifungana mabao mawili *KWA* sita.

[C] hutumika katika nahau na misemo mbalimbali: *-enyewe kwa -enyewe* (ona *-enyewe*); *moja kwa moja* (ona moja); *kwa hali na mali* (ona hali); *bega kwa bega* (ona bega).

Chini ya vidahizo *-enyewe, moja, hali na bega* misemo iliyoandikwa kwa italiki chini ya kidahizo *KWA* inaweza kupatiwa maelezo au mifano ya matumizi kama inavyoonekana hapa chini:

- enyewe kv ... -enyewe kwa -enyewe* (ms) walipigana wenyewe *KWA* wenyewe;
moja ji ... *moja kwa moja* (ms) aliposikia taarifa ya habari aliondoka moja *KWA* moja hadi kwa wazi wake;
hali ji ... *kwa hali na mali* (ms) marafiki zake waliungana naye kwa hali na mali wakati wa matatizo yake;
bega ji ... *bega kwa bega* (ms) wanakijiji walishirikiana bega kwa bega katika kufanya kazi za maendeleo ya kijiji chao.

MSAMIATI

ainisha	- classify
akisi	- reflect
ambua	- deplete
dhima	- obligation
jikita	- be established
urejeleaji	- reference
kiambata	- collocation
kiambata huru	- free collocation
kiambata thabiti	- fixed collocation
kibadala	- substitute

⁴ *ku* = kiunganishi

⁵ *kh* = kihusishi

kidahizo	- an entry
kipashio	- constituent
maana changilizi	- compositional meaning
maana leksika	- lexical meaning
nduni	- characteristic(s)
uribiti	- fixity
utenge	- irregularity

MAREJEO

Bakhressa, S.K. 1992.

Kamusi ya Maana na Matumizi. Nairobi: Oxford University Press.

Johnson, F. 1939.

A Standard Swahili-English Dictionary. Nairobi, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. 1981.

Kapinga, M.C. 1983.

Sarufi ya Maumbo ya Kiswahili. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Khamisi, A.M. 1993.

Taarifa za Kisarufi Katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Warsha ya Kanda Juu ya Kusahihisha Kamusi ya Kiswahili Sanifu: Kibaha, 16-20 Agosti 1993.

Landau, S.I. 1984.

Dictionaries - The Art and Craft of Lexicography. New York: The Scribner Press.

Zgusta, L. 1971.

Manual of Lexicography. The Hague: Mouton.